Kanisa Tunalolitii

(The Church We Honor)

Na

Ellis P. Forsman

Kanisa Tunalolitii

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Kanisa Tunalolitii

Efe. 5:27

Efe. 5:27, "*Apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa.*"

Kanisa la Kristo ni kubwa kuliko taasisi zote za wanadamu.

Kwa sababu Mungu ndiye mwanzilishi.

Efe. 3:10-11, "*Ili sasa kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu war oho; kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Bwana wetu.*"

Kwa sababu Kristo ndiye mjenzi.

- Mat. 16:18, "*Nami nakuambia wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.*"
- Zab. 127:1, "*BWANA asipoijenga nyumba waijengao wafanya kazi bure. BWANA asipoulinda mji yeye aulindaye akesha bure.*"

Kwa sababu Kristo ndiye kichwa chake.

Kol. 1:18, "*Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanissa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu,ili kwamba awe mtangulizi katika yote.*"

Kwa sababu Kristo ndiye Mwokozi.

Efe. 5:23, "*Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa chaa kanisa; naye ni mwokozi wa mwili.*"

Hivyo, tunapaswa kuwa na dhana sahihi kuhusu, na shukurani juu ya kanisa.

Matamshi kadhaa zimetumika kwenye Agano Jipya ili kuliwakilisha kanisa. Ebu tuangalie vichache.

Kanisa kama jengo

1 Kor. 3:9, "*Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu; ninyi ni shamba la Mungu, ni jengo la Mungu.*"

Hapa tunaona uimara wake.

Lina msingi imara na usiotikisika.

1 Kor. 3:11, "*Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani Yesu Kristo*."

Milango ya kuzimu haitalishinda.

Mat. 16:18, "*Nami nakuambia wewe ndiwe Petro na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.*"

Limeundwa kwa vitu tofauti na vifaa vingi.

Neema ya ajabu na kweli iliwatoa katika shimo la dunia.

Kol. 1:13-14, "*Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani msamaha wa dhambi.*"

Vifaa hivi "*vinaungamanisha.*"

Efe. 2:21, "*Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana.*"

Ni maskani ya kweli ya Mungu.

Efe. 2:22, "*Katika yeye ninyi nanyi mmejengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho.*"

Hivyobasi kanisa ni jengo la kiroho.

1 Pet. 2:5, "*Ninyi nanyi kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo.*"

Leo hii kuna makanisa mengi sana ambayo ni ya hovyo kuliko lile lililoanzishwa na Bwan na Mwokozi Yesu Kristo.

Kanisa kama mwili

Hapa tunaona umoja wake na ushirika.

Uhusiano wa Kristo kwa kanisa – Yeye ndiye kichwa chake halisi.

Kol. 1:18, "*Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanissa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu,ili kwamba awe mtangulizi katika yote.*"

Uhusino wa Kristo kwa Wakristo – Ni mwokozi wa mwili.

Efe. 5:23, "*Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa; naye ni mwokozi wa mwili.*"

Uhusiano wa Wakristo kwa kilaa mmoja – "ni viungo kwa kila mmoja."

Rum. 12:5, "*Vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo kila mmoja kwa mwenzake.*"

Umoja wa mwili.

1 Kor. 12:12, "*Maana kama vile mwili mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo.*"

Katika kifungu hiki tunakumbushwa kwamba zawadi na karama miongoni mwa viungo vya mwili wa Kristo hufanya kazi kama viungo vya mwili wa damu na nyama.

Lango la kuingia katika mwili.

- 1 Kor. 12:13, "*Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja.*"
- Yoh. 3:3-5, "*Yesu akajibu akamwambi, amin, amini, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa mara ya pili hawezi kuuona ufalme wa Mungu. Nikodemo akamwambia awezaje mtu kuzaliwa akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? Yesu akajibu, amin, amini nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hwezi kuuingia ufalme wa Mungu.*"

Kwa mafundisho ya Roho sote tunabatizwa katika Kristo.

Maelewano ya mwili.

1 Kor. 12:25-27, "*ili kusiwe na faraka katika mwili, bali viungo vitunzane kila kiungo na mwenzake. Na kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia nacho, kiungo kimoja kikitukuzwa viungo vyote hufurahi pamoja nacho. Basi nili mmekuwa mwili wa Kristo, naa viungo kila mmoja peke yake.*"

Kila kiungo kinamuundo wake, sehemu, na matumizi. Hata vile vinyenyekevu huunda sehemu ya mwili.

1 Kor. 12:15, "*Mguu ukisema kwa kuwa mimi si mkono, mimi si wa mwili; je! Si wa mwili kwa sababu hiyo?*"

Kanisa kama shamba la mizabibu

Mat. 20:1, "*Kwa maana ufalme wa mbinguni umefanana na mtu mwenye nyumba aliyetoka alfajiri kwenda kuajiri wakulima awapeleke katika shamba lake la mizabibu.*"

Hapa tunaona inafanya kazi. Ebu tuangalie vitu vinne alivyosema Yesu:

Mwenye nyumba aliamka "*asubuhi na mapema.*"

Hii inaonyessha umuhimu wa kazi. Hakuna kitu muhimu kama kazi ya Bwana.

Mat. 6:33, "*Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*"

Mwenye nyumba alikwenda "*kuajiri.*"

Hakuwalazimisha kuingia katika shamba lake la mizabibu; hata sisi tusijaribu kuwaingizaa watu kanisani kwa kuwalazimisha. Anawatafuta watu wanaoweza kujitolea; hamvuti mtu katika kazi yake.

Mwenye nyumba alikwenda "*kuajiri wafanya kazi.*"

Hakuwataka wachovu au wadhaifu; wanapaswa kuwa wafanya kazi. Hapendi wafanyakazi wake wawe wavivu.

Mwenye nyumba alikwenda "kuajiri wafanyakazi katika shamba lake la mizabibu.

Inaleta tofauti palipofanyika kazi; wengi hufanya kazi nzuri, lakini katika sehemu isiyo sahihi. Wengine hudhani hakuna tofauti, lakini kama kazi yetu mbele za mungu inapaswa kupewa thawabu ya milele, lazima ifanyike katika ufalme wake.

- Mat. 7:21, "*Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.*"
- Kol. 3:17, "*Na kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yote.*"

- Efe. 3:21, "*Naam, atukuzwe katika kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote na milele na milele. Amina.*"

Kanisa kama bibi harusi

Hapa tunaona usafi wake.

Hatua za kuolewa kwa Kristo.

Unapofikiria kuhusu kanisa kama ufalme, katika swaala la wokovu, unafikiria kuhusu swala la kuwa mwanchi katika ufalme wa Mungu.

Unapofikiria kanisa kama familia, katika wokovu, unafikiria kuzaliwa mara ya pili, ya kuwa mwana wa Mungu.

Ndivyo ilivyo, unapofikiria kanisa kama bibi harusi wa Kristo, katika mfumo wa uongofu, unafikiri kuhusu ndoa.

Kwanza ni lazima umwamini Yesu Kristo.

- Yoh. 8:24, "*Kwaiyo naliwaambieni yaa kwamba mtakufa katika dhambi zenu; kwa sababu msiposadiki ya kuwa mimi ndiye, mtakufa katika dhambi zenu*."
- Heb. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao.*"

Alafu lazima ugeukie toba kutoka katika maisha ya zamani.

- Luka 13:3, "*Nawaambia, sivyo; lakini msipotubu ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo.*"
- Mdo. 17:30, "*Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu.*"

Laazima ufanye kiapo chaa imani yako katika jina la Yesu Kristo.

Mdo. 8:36-37, "*Wakawa wakiendelea njiani wakafika mahali penye maji; yule towashi akasema tazama maji haya; ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana. Akajibu akanena, naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu.*"

Alafu tendo la ubatizo kaatika jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu inamaliza sherehe hii. Ndoa haiwezi kukamilika mpaka sherehe ya ubatizo.

Kristo ana bibi harusi mmoja tu – kanisa .

Yesu anakataa mitara.

Mat. 19:9, "*Nami nawaambia ninyi, kila mtu atakayemwacha mkewe, isipokuwa kwa sababu ya uasherati, akaoa mwingine, azini; naye amwoaye yule aliyeachwa azini.*"

Je Yesu alihubiri jambo moja na kufanya lingine? Je alizungumzia wake wengi?

- Mdo. 4:10-12, "*Jueni ninyi nyote na watu wote wa Israeli ya kuwa kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulubisha na Mungu akamfufua katika wafu, kwa jina hilo mtu huyu anasimama ali mzima mbele yenu. Yeye ndiyee jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni. Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*"
- Mdo. 20:28, "*Jitunzeni nafsi zenu na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.*"

Kama bibi harusi awakataavyo wengine wote na kuwa kwa mumewe pekee, na kwake tu, ndivyo kanisa linavyopaswa kujiweka kwa Kristo na kwake tu.

Hivyo, kanisa linapaswa kujitenga na dunia.

- Rum. 12:2, "*Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu.*"
- 2 Kor. 6:14-17, "*Msifungiwe nira na wasioamini, kwa jinsi ilivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gaani kati aya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza? Tena pana shirika gani kati ya Kristo na Beliari? Au yeye aaminiye ana sehemu gani pamoja naa asiyeamini? Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aaliye hai; kama Mungu aalivyosema ya kwamba nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. Kwa hiyo tokeni kati yao, mkatengwe naao asema Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu, nami nitawakaribisha.*"

Hatupaswi kuwa sehemu ya dunia, au kutaniana na dunia.

1 Yoh. 2:15, "*Msiipende dunia wala mambo yaliyomo katika dunia, mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake.*"

Hapa kwenye msemo huu zaidi tunaona usafi wa kanisa ukionyeshwa.

Efe. 5:27, "*Apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa.*"

Kanisa linapaswa kuwa safi kwa sababu uhalisia na tabia ya kanisa linahitaji usafi wake.

Kila mtu aanayekuja kanisani anafanywa kuwa safi kwa damu ya Mwana –kondoo.

- 1 Pet. 1:18-19, "*Nanyi mfahamu kwamba mlikombelewa si kwa vitu viharibikavyo, wala fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa yaani, ya Kristo.*"
- Ufu. 1:5, "*Tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanzaa wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia. Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake.*"

Kanisa linapaswa kuwa safi kwa sababu ya ununuzi wa gharama.

- Mdo. 20:28, "*Jitunzeni nafsi zenu na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.*"
- Efe. 5:25, "*Enyi waume wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa akajitoa kwa ajili yake;*"

Kanisa linapaswa kuwa safi kwa sababu wokovu wa waliopotea unauhitaji.

Mat. 5:13-16, "*Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu. Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu yam lima. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu yaa kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.*"

Mvuto ni kitu ambacho sote tunayo.

Rum. 14:7, "*Kwa sababu hakuna mtu miongoni mwetu aishiye kwa nafsi yake, wala hakuna afaye kwa nafsi yake.*"

Mvuto wetu unaweza kuwa mbaya au mzuri, lakini siyo vyote.

Mat. 12:30, "*Mtu asiye pamoja nami yu kinyume change; na mtu asiye kusanya pamoja nami hutapanya.*"

Kanisa linapaswa kuwa safi kwa sababu ya umoja wake na Kristo.

Tunaunganishwa na Kristo.

- 1 Kor. 12:27, "*Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila mmoja peke yake.*"
- Efe. 5:30, "*Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake.*"

Itakuwa upumbavu kuvitoa viungo vya Kristo kwa ajili ya dhambi.

1 Kor. 6:15-16, "*Je! Hamjui ya kuwa miili yenu ni viungo vya Kristo? Basi nivitwae viungo vya Kristo na kuvifanya viungo vya kahaba? Hasha? Au hamjui ya kuwa yeye aliyeungwa na kahaba ni mwili mmoja naye? Maana asema wale wawili watakuwa mwili mmoja.*"

Kwa vile sisi ni bibi harusi wa Kristo, matawi katika mzabibu, wanafunzi wa mkubwa, uhusiano huu unatoa utengano na dunia.

Kanisa linapaswa kuwa safi kwa sababu ya hatima yake.

- Ufu. 19:7-9, "*Na tufurahi tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa harusi ya Mwana-kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari. Naye amepewa kuvikwa kitani kizuri, ing'arayo, safi, kwa maana kitani nzuri hiyo ni matendo haki ya watakatifu.*"
- Ufu. 21:27, "*Na ndani yake hakitaingia kamwe chochote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-kondoo.*"

Mbinguni hakutakuwa na wivu, uchafu, masengenyo, kiburi, ubatili, au dunia.

Hitimisho

Kifungu chetu kinasema kwamba Kristo anakuja kuwapokea wale walioishi maisha ya utakatifu na safi.

Bibi harusi wake hatakuwa mwenye dhambi, wa kidunia, mchafu, au watu wachafu.

Wazo hili linapaswa kutufanya kila mmoja wetu kuamua upya anavyoweza kuishi ili kwamba Bwana apendezwe kummiliki atakapokuja tena.

Kwa kila Mkristo Paulo anasema, "*ujilinde nafsi yako uwe safi.*"

1 Tim. 5:22, "*Usimwekee mtu mikono kwa haraka, wala usizishiriki dhambi za watu wengine. Ujilinde nafsi yako uwe safi.*"

Kwa kila kusanyiko Paulo anasema,

2 Kor. 11:2, "*Maana nawaonea wivu, wivu wa Mungu; kwa kuwa naliwaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi.*"